



NAETISL

National Association of
Educational Translators and
Interpreters of Spoken Languages



MODDC

Missouri
Developmental
Disabilities Council

Kuelewa Tathmini ya Elimu Maalum: Mwongozo wa Mzazi

Funding for the Supporting Language Access in Schools Project in Missouri provided by the Missouri Developmental Disabilities Council, was supported by the Administration for Community Living (ACL), U.S. Department of Health and Human Services (HHS) as part of a financial assistance award totaling \$1,361,246 with 100 percent funding by ACL/HHS. The contents are those of the author(s) and do not necessarily represent the official views of, nor an endorsement, by ACL/HHS, or the U.S. Government.



naetisl@gmail.com

NAETISL



Follow us



MODDC



moddc@moddcouncil.org



www.naetisl.org

www.moddcouncil.org



Kuelewa Tathmini ya Elimu Maalum: Mwongozo wa Mzazi

Tathmini ya elimu maalum ni nini?

Tathmini ya elimu maalum inafanywa ili kubaini kama mtoto wako ana ulemavu na anaweza kufaidika na huduma maalum za elimu. Tathmini ni seti ya majaribio, uchunguzi na mahojiano ambayo husaidia kuelezea utendaji wa mtoto wako na jinsi anavyojifunza vyema zaidi. Lazima utoe idhini yako kwa tathmini.

Je, Watoto wote hufanyiwa tathmini moja?

Hapana, tathmini ni tofauti kwa kila mtoto kulingana na matatizo ya mtoto katika kujifunza. Watoto wengi watajaribiwa uwezo wao wa kiakili na, ikiwa wana umri wa kutosha, juu ya ujuzi wao wa jumla wa kitaaluma. Lakini majaribio ya usemi na lugha, ujuzi wa kutumia viungo vya mwili, tabia, usomaji, hesabu, na maeneo mengine yanaweza kujumuishwa inapohitajika. Pia ni kawaida kwa wazazi kuhojiwa kuhusu historia na maendeleo ya mtoto.

Ni nani anayehusika katika mchakato wa tathmini?

Wataalamu kadhaa hushirikiana kama timu kueleza uwezo na changamoto za mtoto wako:

- **Mwanasaikolojia wa Shule**

- Hufanya majaribio ya kiakili na kitaaluma ili kuona jinsi mtoto wako anavyojifunza na kufikiri.
- Huchunguza tabia ya mtoto wako na ujuzi wa kutatua matatizo.
- Husaidia kuamua kama matatizo ya kujifunza au tabia yanahusiana na ulemavu.



- **Mtaalamu wa Magonjwa ya Usemi na Lugha (SLP)**
 - Hutathmini jinsi mtoto wako anavyoelewa na kutumia lugha.
 - Hutathmini uwazi wa usemi, msamiati, sarufi na matumizi ya lugha katika jamii.
 - Hubainisha iwapo changamoto za mawasiliano huathiri ujifunzaji au mwingiliano wa kijamii.
- **Mwalimu wa Darasani**
 - Hushiriki uchunguzi kuhusu jinsi mtoto wako anavyojifunza, kushiriki, na tabia yake darasani.
 - Hutoa mifano ya kazi za shule.
 - Husaidia timu kuona jinsi ujuzi wa mtoto wako ulivyo, ukilinganishwa na matarajio ya kiwango cha daraja.
- **Mfanyikazi wa Kijamii**
 - Anaweza kumhoji mtoto wako na familia ili kuelewa mambo ya kijamii, kihisia, au ya nyumbani ambayo huathiri kujifunza.
 - Husaidia kutambua uwezo, mafadhaiko, na usaidizi nje ya shule.
 - Hutoa utambuzi katika mahusiano ya rika na ustawi wa kihisia.
- **Wataalamu wengine (wanapohitajika)**
 - **Mtaalamu wa tiba ya Kazi:** Huangalia ujuzi wa kutumia viungo vidogo vya mkono, mwandiko, na mahitaji ya hisia.
 - **Mtaalamu wa Tiba ya Kimwili:** Huangalia usawa, uratibu, na harakati.
 - **Muuguzi/Mtaalamu wa Afya:** Hukagua historia ya matibabu ambayo inaweza kuathiri kujifunza.
 - **Mtathmini wa Lugha Mbili:** Huhakikisha kuwa majaribio ni sawa kwa wanafunzi wanaozungumza zaidi ya lugha moja





- **Wazazi na Watu Wengine wa Familia**

- Hutoa historia ya mambo kadhaa ikiwa ni pamoja na afya ya mtoto, ukuaji wa awali, tabia, elimu ya awali, nyumba ya familia, lugha.
- Hushiriki wasiwasi wake kumhusu mtoto.

Je taarifa hukusanywa kwa njia gani?

- **Majaribio:** Majaribio yanayolingana hupima ujuzi katika maeneo kama vile kusoma, hesabu, kumbukumbu, lugha au ujuzi wa kutumia vidole.
- **Uchunguzi:** Wataalamu hutazama mtoto wako darasani au katika mazingira mengine ya shule.
- **Mahojiano na Hojaji:** Wazazi, walimu, na wakati mwingine mwanafunzi hushiriki mitazamo yao.
- **Mapitio ya Rekodi:** Kadi za ripoti za awali, rekodi za afya na matokeo ya awali ya mtihani huzingatiwa.

Nitapataje matokeo?

Timu ya tathmini itakutana nawe ili kukagua matokeo yote.

Unapaswa kuuliza maswali, kuomba maelezo, na kushiriki mtazamo wako. Una haki ya kupokea taarifa hii katika lugha yako ya nyumbani ikiwa hujui Kiingereza vizuri. Uliza huduma za mkalimani au mfasiri ili uelewe vyema matokeo ya majaribio na mapendekezo

Utapokea ripoti iliyoandikwa ambayo inaelezea:

- Iwapo mtoto wako anahitimu kupata elimu maalum chini ya mojawapo ya kategoria za IDEA.
- Nguvu na changamoto za mtoto wako.
- Mapendekezo ya usaidizi na huduma.





Nini hufanyika baada ya tathmini?

Mtoto wako akipatikana kuwa anastahili, timu—ikiwa ni pamoja na wewe—itatayarisha Mpango wa Elimu ya Mtu Binafsi (IEP) unaobainisha malengo na huduma. Ikiwa mtoto wako hastahiki, shule itajadili usaidizi mwingine ambao unaweza kusaidia.

Kumbuka : Tathmini haihusu kuweka lebo—inahusu kuelewa mahitaji ya mtoto wako ili aweze kuendelea na kujifunza.

Bado una maswali?

Onge ana meneja wa kesi wa mtoto wako ama mshirika yeyote watimu ya tathmini.

How can I get help in my language?

Omba huduma za mkalimani katika shule ya mtoto wako au katika ofisi za wilaya ya shule. Omba taarifa iliyotafsiriwa na kuandikwa iwapo utaihitaji. Taarifa inayopatikana kwa wazazi wote katika wilaya ya shule inafaa kupatikana kwako pia.

